



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Wednesday, 26th July, 2023
Third Assembly – Forty Ninth Sitting

*[The County Assembly met at 2:35p.m. at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Honourable Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Members have your seats. Clerk?

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

Honourable Members, the County Assembly is privileged to welcome students and teachers from Free Town Primary School. I will name one by one, if you hear your name please stand up and bow:

1. *Derick Odhiambo*
2. *Rashid Daudi,*

The former heavy weight champion...

3. *Michael Tyson*

[Applause]

4. *Yusuf Khamis*
5. *Lucas Kaingu*
6. *Jamal Yusuf*
7. *Briton Kiplagat*
8. *Yusuf Idd*
9. *Alex Nzombo*
10. *Alex Achieng*
11. *Joseph Kazungu*
12. *Hamza Ziro*
13. *Brian Baraka*
14. *Issa Karim*
15. *AbdulRahim Mohammed*
16. *Raphael Chiroo*

17. *Moses Mogela*
18. *Lyversion Mwadime*
19. *Ibrahim Kazungu*
20. *Frank Jacob*
21. *Hashim Kaingu*
22. *Evans Musyoka*
23. *Lucky Ranny*
24. *Wilfred Kathuri*
25. *Fatma Neema*
26. *Jackline Murithi*
27. *Diana Odhiambo*
28. *Frida Mbodze*
29. *Mwanamisi Kengan*
30. *Asha Matano*
31. *Mariam Cosmas*
32. *Suhaila Afan*
33. *Siti Hamza*
34. *Nuru Mohamed*
35. *Mariam Kahindi*
36. *Asia Suleiman*
37. *Aisha Bwanahaji*
38. *Wendy Adhiambo*
39. *Monica Alfred*
40. *Kingstone Mutugi*
41. *Funnuel Anyika*
42. *Jeremy Samson*
43. *Peter Vuko*
44. *Hussein Martinez*
45. *Suleiman Omar*
46. *Jared Nyambu*
47. *Victor Kombe*
48. *Emmanuel Wekesa*
49. *Levis Light*
50. *Ramadhan Ibra*
51. *Abdalla Sheban*
52. *Abdalla Nassor*

Any other Member who has not heard his or her name?

[Silence]

You can just stand up and bow...

[Applause]

Sorry, I will continue reading the names...

53. *Salma Salim*

54. *Claris Pili*
55. *Mariam Yusuf*
56. *Aisha Athman*
57. *Saum Anzanzi*
58. *Veronica Kalechi*
59. *Halima Swaleh*
60. *Cynthia Yaya*
61. *Amina Dama*
62. *Faith Chelangat*
63. *Salome Baya*
64. *Fathma Mohamed*
65. *Dorcas Luvuno*
66. *Celine Wangari*
67. *Purity Chepkemoi*
68. *Fadhat Hassan*
69. *Hidaya Bure*
70. *Agnes Bahati*
71. *Janet Malombo*
72. *Mariam Kadii*
73. *Furaha Mbuche*
74. *Holiness Philip*
75. *Mariam Mohamed*
76. *Rachael Wanje*
77. *Jorge Mberi*
78. *Binti Nassir*
79. *Rariina Kombe*
80. *Nasra Juma*
81. *Zeituni Kazungu*
82. *Lucy Muholeli*
83. *Cycelia Kadzo*
84. *Salima Mwaka*
85. *Kibibi Bahati*
86. *Salma Alfan*
87. *Mathew Francis*
88. *Mbarak Swaleh*
89. *David Kombe*
90. *Jeremy Joshua*
91. *Anton Mwala*
92. *Kelvin Chengo*
93. *Hamsi Amani*
94. *Baraka Jackson*

And last but not least...

95. *Isiah Gitonga*

[The students and teachers rose and bowed]

Welcome once again to the County Assembly of Mombasa and I will let the Honourable Member from Frere Town Ward to give a welcoming remark. Yes, Honourable Mariam?

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii niweze kukaribisha watoto wangu wa Frere Town Primary School. Waheshimiwa wenza, leo tumekuwa na bahati kuu maana yake hii ni timu nyengine, asubuhi tumekuwa na watoto wa Frere Town 86 na hivi sasa tuko na watoto wa Frere Town 84 jumla wamekuja watoto 170. Kwa hivyo mimi wasichana wangu, vijana wangu, na walimu wa Frere Town karibuni sana katika Bunge la Kaunti yetu ya Mombasa, ni pahali ambapo nyinyi pia mutaweza kujifunza mengi muweze mukirudi kule shule muweze kuwaambia wanafunzi wenzenu yalo mumeweza kusoma leo hapa, yale mumeona hapa vile viongozi wenu ama mimi mama yenu tunavyofanya kazi hapa kwa Bunge. Kwa hivyo mimi nimefurahi sana kuona sura zenu na ni saa nane ndio nataka muwe *attentive* muweze kusikiza vizuri muweze kuelewa ni nini kinaendelea hapa. Imani yangu ni moja, Frere Town ni Wadi ambayo tuko mbele sana kung'ang'ana na maisha, kwa hivyo mimi kama kiongozi wenu, mama yenu ni imani yangu kwamba siku moja mutaweza kusoma kwa bidii mupite mwende shule za upili mufike vyuo vikuu na *In Shaa Allah* katika hilo kundi lenu iwe kutakuweko wengi wenu ambao wataingia katika hili Jumba ama Bunge hili na wao waweze kuwahudumia watu wetu wa Frere Town. Kwa hivyo mimi nawapenda sana, nimefurahi sana kwa kuja kwenu; karibuni na mjisikie muko nyumbani asanteni sana. Ahsante Bwana Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Mariam Baimu, MCA Frere Town Ward. Yes, Leader of Majority?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa niaba ya Bunge hili la Mombasa kuwakaribisha wanafunzi wetu katika Jumba hili katika mojawapo ya taratibu na mpangilio wa wao kujifunza na kuweza kuyakinisha yale ambayo wanayasoma kwenye madaftari lakini leo kuyashuhudia wanapozungumzia masuala ya serikali, wanapozungumzia masuala ya Ugatuzi, wanapozungumzia masuala ya Wawakilishi Wadi, leo wako ana kwa ana na Wawakilishi Wadi kutoka kata mbali mbali katika Jimbo letu la Mombasa. Mheshimiwa Spika, pia niwausie tu wanafunzi hawa ya kwamba kwenda shule si kwa kusudio la ufanisi pekee lakini ni njia mojawapo ya kuondoa ujinga katika maisha na kufungua mianya mingi ambayo ni ya natija katika jamii yetu. Vile vile Mheshimiwa Spika pia niwausie vijana hawa ya kwamba uwepo wao katika madarasa yale kule shuleni kuna wakinga na mengi ambayo ni ya masaiibu huku nje, huku nje hali si hali na wao wenyewe watakuwa na mfano bayana kwa wale wakubwa zao ama maharimu wao ambao waliachishwa shule kabla wakati unaostahiki hali ilivyo kule nje. Sasa hivi kwa mzazi ana kila sababu ya kujua mwanae kala nini akijua anaenda shule, anajua mwanae akitoka shule atakula nini kwa sababu anajua katoka shule lakini pindi anapotoka nje ya majengo ya shule Mheshimiwa Spika akichelewa kwa maandalizi ya shule basi hesabu yake haipo, anapototeleka mzazi hana habari ya kwamba huyu yuko wapi anakula nini? anavaa nini?!

Kwa hivyo uwepo wao katika kile kivuli cha madarasa hiyo ni sababu chanya kwao kumakinika, kuzingatia yale waliyoyaandea kule Mheshimiwa Spika ili wawe faraja kwao binafsi, faraja kwa wazazi wao, faraja kwa jamii pindi watakapohitimu katika masomo yao yote hadi yale ya ngazi ya juu kopna kuja kuwa mchango katika jamii na kufika pale ambapo sisi tuliwatangulia tutakuwa tumewakwamilia na wao kusongeza mbele katika ufanisi wa Jamhuri yetu ya Kenya lakini zaidi Gatuzi la Mombasa na pale maeneo ya Frere Town wanapotoka. Ahsante Mheshimiwa Spika na niwakaribishe kwa moyo mkunjufu katika maeneo yetu ya Bunge. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Clerk next Order please?

STATEMENTS

HARASSMENT OF BOAT OPERATORS AND BEACH TRADERS AT BAMBURI PUBLIC BEACH

Yes, Honourable Abdirahman Abdulkadir, Chairperson Committee on Tourism, Culture and Trade or any other Member from that Committee? I can see that Honourable Hamisi Mbaya is up. Yes, Honourable Hamisi Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii ambayo ilikuwa rasmi iweze kupeanwa ripoti ama *Statement* kutoka kwa Mwenyekiti lakini kwa bahati nzuri na mipango ya Mwenyezi Mungu kwa saa hii hayupo kwa hiyo mimi kama Mwanachama nitaomba kuongezewa muda takriban kama wiki tatu hivi tutakuwa na maelezo kamili. Ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): As per your statement you said that the Chairman is not around so I will give you one week please respond to this Statement as it has been pending in this Honourable House quite a long time, so Honourable Hamisi Mbaya plus your Committee we are giving you one more week.

Hon. Hamisi Mbaya: Ilikuwa naomba isiwe wiki moja Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Hamisi...

[Interruption]

Hon. Hamisi Mbaya: Naomba...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): ...It has been pending for quite a long time so we are giving you and your Committee one week.

Hon. Hamisi Mbaya: Okay thank you Sir.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes Clerk?

BLOCKAGE OF PUBLIC ACCESS ROAD NEAR KIEMBENI BAPTIST CHURCH

Yes, Honourable Amriya Juma Boy, Chairperson Committee on Lands, Housing and Urban Planning please respond to the Statement.

Hon. Amriya Juma: Thank you Mr. Speaker, good afternoon. Mr. Speaker, I am here to report that we are yet to receive the correspondence from the Ministry of Lands and Urban Planning so we are requesting seven days so that we can come up with the necessary response. Thank you for your indulgence.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Okay one week is granted. Yes Clerk?

STATUS OF LAND OWNERSHIP IN KASHANI, BAMBURI WARD

Yes, Honourable Amriya Boy Juma please respond to the Statement on Status of land ownership in Kashani, Bamburi Ward.

Hon. Amriya Juma: Thank you Chair. So, the Committee is also requesting your indulgence to see that we get the correspondence in time so that we are requesting seven days to have the response on the status of the land ownership in Kashani, Bamburi Ward so we have the same prayers your Chair grant us several more days we shall avail the response in time. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Amriya. Honourable Patrick Mbelle before you respond do you have any issue pertaining the response from Honourable Amriya.

Hon. Mbelle: Thank you Mr. Speaker, although I feel dissatisfied by the answer of our able Chair for the Committee of Lands but I also agreed to grant her the seven days so that we can get the satisfied answer although temperatures in the said piece of land are still high and we are living in fear. So, I asked that the seven days be done justice so that we get an answer on those seven days. Thank you, Honourable Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu): Thank you. Honourable Amriya, the seven days are granted so we would like your Committee to bring back the response to this House in a weeks' time.

Hon. Amriya Juma: I am so obliged.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu): Yes Clerk?

STATUS OF MWAKIRUNGE DUMPSITE

Yes, Honourable Juma Mwalimu Chairperson Committee on Environment Energy and Solid Waste Management, status of Mwakirunge dump site.

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa sababu zisizoepukika, bado hatujapata majibu kwa heshima yako Mheshimiwa Spika naomba siku kumi na nne tafadhali.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Chair, Committee on Environment Energy and Solid Waste Management, the issue on the Mwakirunge dump site has also been pending in this House, the Honourable Member from Mwakirunge has been looking for the same response so we will grant you one week. So, in a weeks' time please make sure you and your Committee make sure you respond back to this Honourable House. Yes Clerk?

COMMUNITY HEALTH POLICY IN THE COUNTY

Yes, Honourable Ogutu or any other Member from Health Committee. Yes, Honourable Frankline Makanga?

Hon. Makanga: Thank you Mr. Speaker Sir. On behalf of the Chair and the Health Committee we wish to seek leave of this Assembly to bring forward the report seven days from today's date.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Okay, permission granted. Yes Clerk?

MOTION

ADOPTION OF REPORT ON THE VETTING OF NOMINEES FOR MEMBERS OF THE COUNTY ASSEMBLY SERVICE BOARD REPRESENTING THE PUBLIC: MR. SWABIR MASOUD AND MS. LYNETTE KAMADI

Yes, Honourable Athman Mwamwiri Vice- Chairperson Committee on Appointments.

Hon. Athman Mwamwiri: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, naomba kujenga hoja ya kupitiswa kwa wawakilishi katika Bodi ya shughuli za Bunge; Bwana Swabir Masoud na Bibi Lynette Kamadi kama ilivyowekwa katika Meza ya Bunge hili siku ya juma nne tarehe 28 mwezi wa saba, mwaka wa elfu mbili na ishirini na tatu. Nimuombe Mheshimiwa Leila, aweze kuunga mkono hoja hii.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Leila?

Hon. Nyache: Ahsante Mheshimiwa Spika. Namesimama kuunga mkono Hoja hii.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Members, I now propose a question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on adoption of Report on the vetting of Member of the County Assembly Service Board representing the public Mr. Swabir Masoud and Ms. Lynette Kamadi be debated in this Honourable House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Leader of Majority.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa sehemu ya kumi na mbili ya sheria za Ugatuzi mwaka elfu mbili na kumi na mbili inapeana fursa kuundwa kwa ushirika katika Bunge hili. Mheshimiwa Spika unapokwenda katika sehemu ya 47(3) arobaini na saba, sehemu ndogo ya tatu inaelekeza pia uwanachama katika ushirika huu wa kusimamia shughuli za Bunge pamoja na kuwa Mwenyekiti na wawakilishi wawili kutoka Bunge hili pia hii sheria imepeana fursa ya mwanamume mmoja na mama mmoja kutoka kwa jamii; wenye uweledi na uzoefu na maswala ya utawala kuwa wanachama katika ushirika huu wa kuendesha shughuli za Bunge. Mheshimiwa Spika, kama Kamati tuliweza kufuata taratibu zinavyo stahiki, kwa mujibu wa sheria zetu za Bunge za uajiri na kutangazia fursa hii watu kutoka kwa jamii ama watu, umma wa kawaida waliweza kuomba nafasi ya kuwakilisha katika ushirika lakini pamoja na yote, uhakiki ulifanya na wawili kati yao wakaibuka ushindi.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 7*

Sisi kama Kamatia tuliweza kuwafanyia uchunguzi wa kina na tukaridhika Mheshimiwa Spika kwamaba tuwafikishe katika Bunge hili ili tuweze kuomba wawakilishi wa Wadi Waheshimiwa wenza kuweza kukubaliana na Ripoti hii na kuwapatia fursa kuwa katika ushirika huu wa shughuli za Bunge. Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia wawili hawa waliwahi kuhudumu kama wanachama wa shughuli za Bunge na vile vile yako mengi chanya ambayo waliweza kufanya katika nafasi ile. Mheshimiwa Spika, kwa mukhtasari tutakubaliana kwamba Bunge hili kwa muda lilisalia na sura ya ki Manispaa lakini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na wawakilishi Wadi wawili katika nafasi zile na hawa wawili katoka umma waliweza kuboresha miundo msingi katika jengo hili. Sasa hivi sote tunajivunia ya kwamba Bunge liko katika sura la Kibunge la kileo kama inavyostahiki na mengi mazuri waliyaafiki ya kwamba wameweka katika mipango na kwa fursa hii itasaidia kwa ushirikiano wa Mheshimiwa Spika kupeleka Bunge letu katika hatua ya kidijitali kama ilivyo sasa hivi. Vilevile Mheshimiwa Spika katika awamu yao pamoja na ushirikiano na kwenye ushirika huu wa shughuli za Bunge waliweza kuweka kanuni ikiwemo mwongozo wa rasilimali watu ambayo kwa muda mwingi haikuwa na sasa hivi tunatarajia taratibu ya kwamba ni jinsi gani watu wataajiriwa na ni jinsi gani watu watapata kupewa mamlaka na kupandishwa daraja kwenye nafasi walizonazo kwa mapangilio na sio kwa upendeleo. Vilevile Mheshimiwa Spika pia waliweza kueka kanuni za usimamizi wa ofisi za nyanjani za Wawakilishi Wadi ya kwamba ofisi itasimamiwa vipi, italipwa vipi itakuwa ikiendeshwa kwa harakati gani pasi na ile kwamba watu wanabebana kihobelabela kwa maridhio ya mtu lakini kuna kanuni makhsusi kwa minajili ya hayo.

Mheshimiwa Spika pia kwa miaka ya nyuma tutakubaliana ya kwamba Bunge hili inapokuja Ripoti za mkaguzi mkuu wa mahesabu tulikuwa tukiwa kwa Ripoti ambayo ni wataalamu wanasema ni *disclaimer* ama Ripoti ya kukanusha. Mheshimiwa Spika katika Ripoti hiyo ilikuwa inaweka sura mbaya katika Bunge letu lakini chini ya Mheshimiwa Spika kama Mwenyekiti na hao wakiwa katika Bodi ile tunajivunia kwamba miaka mitano iliopita Ripoti za Mkaguzi wa Mahesabu haukufika katika daraja la A lakini tulikuwa katika nafasi ya pili ya Ripoti ambayo ni Ripoti yenye sifa wataalamu wa mahesabu wakaita *qualified Report* ambayo kwetu imetujenga na kuweka hadhi ya Jumba hili. Kwa ushirikiano wao huo tukakuta ni bayana sisi katika Kamati hii na kwa jinsi walivyoweza kujieleza kupatia fursa nyengine tena Mheshimiwa Spika kuweza kutuchukua pale waliposazia na kuweza kusonga mbele zaidi kuweza kuliboresha na kujenga hadhi zaidi kwa jumba hili Mheshimiwa Spika. Kwa hayo mengi Mheshimiwa Spika niwaombe Waheshimiwa kwa heshima na taadhima ya kwamba tuafiki Ripoti hii ya kuweza kuwapitisha wawili hawa wakiwa ni wakilishi kutoka kwa jamii mama mmoja na baba mmoja kwa jina la Swabri Masoud na Lynette Kamadi kuweza kusukuma gurudumo hili la huduma za shughuli za Bunge. Ahsante Mheshimiwa Spika na niombe Waheshimiwa wenza waweze kuunga mkono Ripoti hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you the Leader of Majority. Yes Honourable Amriya Boy Juma?

Hon. Amriya Juma: Thank you very much Mr. Speaker for according me this opportunity to also contribute to the Motion on the approval of Nominees for the County Public Service Board. Mr. Speaker, as you are aware that I am part of the Appointments Committee and we conducted a very successfully vetting process and the Nominee had all the qualifications in terms of educational background the Nominees had the necessary papers, in terms of degree qualifications and also the necessary requirements from the Ethics and Anti Corruption, clearances from CRB the Committee ensured that the Nominee had all the necessary clearances.

In terms of experiences; we all know that Mrs Lynette Kamadi and Mr. Swabir have formally served in the County Assembly Service Board and they are well versed with our matters as the County Assembly. Also, in the matters that we are constrained with resources and they needed to complete the projects that they had initiated, so the Nominees actually promising on what will be the deliverables in the next five years. So, as a Committee we anonymously agreed that we forward the Report for approval in this Honourable House and I stand here to support their nomination and appointments. Thank you very much.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Amriya. Yes, Honourable Kachumbo Florence?

Hon. Kachumbo: Thank you Mr. Speaker for this opportunity to air my views. I do agree with this Motion for the adoption of the two external Members in the Board, that is County Services Board; Mr. Swabir Masoud and Ms. Lynette Kamadi as Members of the Board we did interview them they are fit for this position and well knowledgeable. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes Mwalimu Juma?

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Bwana Mwenyekiti. Mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu na yote ni kwa sababu ya sifa kochokocho tulizopewa na Kiongozi wa Wengi Bungeni nami kama kiongozi mwenzana sina budi kuwavisha pete na kuunga mkono na kwa sababu ya zile sifa tulizopewa ya kwamba pia wameboresha Jumba hili basi nawaunga mkono ili waweze kuzidi kutuboreshea hili Jumba hususan hapa ndani kuwe kidijitali. Ahsante sana Bwana Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mbelle?

Hon. Mbele: Thank you Mr. Speaker Sir. First of all I want to agree with Majority Leader, that Ms. Lynette Kamadi is an outstanding lady and I would also want to let this House know that she was my High school teacher; she taught me from one to form four and during that time, her ethics and how she taught us was something that I will always remember to date because she made a man out of a boy at that time and this time I would wish to join other Members to support the nomination of these two, the lady and gentleman knowing very well they will at some point be able to take this House to a better level. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Hamida?

Hon. Noor: Thank you Mr. Speaker for giving me the opportunity. I rise to support the Report that has been brought here in front of us for Mr. Swabir Masoud and Ms Lynette Kamadi. Mr. Speaker Sir you are well aware that, they have worked with us in the previous regime and we have seen the kind of work that they have offered for us especially in the Assembly Service Board and with their qualification Mr. Speaker Sir, we have seen that they are qualified for the job that they have been given and we are satisfied with what we have read and seeing this report that is in front of us and with this we are hoping that, they will take us to the next level, for that I do support the Report thank you very much.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Hamid?

Hon. Mohamed Hamid: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa fursa hii. Sina budi ila kukubaliana na wenzangu kwa sababu ya kazi ya hawa ndugu wawili waliokuwa nayo; kwa Ripoti hii iliyokuwa hapa ni watu walioonekana wamefanya kazi kwenye Bunge lililopita. Kwa hivyo wana uzoefu na kazi hii na watasaidia zaidi wale wenzao ambao ni wageni wanaokuja kutoa huduma katika hii Bodi. Kwa hivyo naona itakuwa ni mchanganyiko ambao utakuwa na manufaa zaidi kwa Bunge letu hili. Kwa hivyo naunga hoja hii ahsante sana ndugu Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Hamid. Yes, Honourable Leila?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia. Kwanza nasimama kuunga mkono hoja hii iliyokuja na Mheshimiwa mwenza, mimi kivyangu nitachangia vilivyo kwa sababu nimeona mama hapa na mimi ni mama kwa hivyo Mheshimiwa Spika nimefurahi sana kwa hii Bodi kuweza kuteua hawa watu wawili ambao ni Bwana Swabir Masoud na Lynette Kamadi. Nikielezea ni kwamba ni watu tunawafahamu na pia waliwahi kujumuika na kufanya kazi katika Kaunti yetu hii ya Mombasa; ni watu tunajua kazi zao na tukiangalia vigezo hapa ni wasomi wamehitimu kabisa, hizi tajriba zao ni za kueleweka. Kwa hivyo mimi ningomba Jumba hili Mheshimiwa Spika waweze kuunga mkono hoja hii tuweze kupata wenzetu wengine katika hii *County Assembly Service Board* ambapo wataeza kusaidia kazi nzuri sana na pia nataka niunge mkono niwapongeze Kamati waliopiga msasa hawa watu wawili ikiongozwa na Mheshimiwa Spika wetu maadamu Spika yuko pale tunajua hawa ni watu wa kisawasawa kwa sababu Mheshimiwa Spika ni mchapa kazi na anaelewa kazi yake vizuri sana. Ahsante Mheshimiwa Spika na nasimama kuunga mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Shuhudia?

Hon. Shuhudia Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika mimi pia nimesimama kuunga mkono hoja hii. kwa sababu nimesikia hapa mimi kibinafsi siwajui lakini nimesikia sifa kochokocho wakimiminiwa. Kwa hivyo pia mimi naunga mkono swala hili la kuwa wao pia wawe katika hio kamati ya katika hio Board. Kwa hayo mengi nashukuru Mhe.Spika. Ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Frankline Makanga?

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi nasimama kuunga mkono kuteuliwa kwa hawa waungwana wawili. Mheshimiwa Spika, tukianza na Bwana Swabir Masoud Abdalla mimi nimeweza kufuatilia historia yake katika Ripoti hii na nikagundua ya kwamba yeye ndio Mhasibu mkuu wa *Interpel*, kampuni ambayo iko katika Wadi yangu eneo la Chaani na kama tunavyo jua kampuni ile kwanza katika utenda kazi wao pamoja na vile wanaisadia jamii ya wana Chaani na yeye ndiye ako katika usukani wa maswala ya fedha pale amedhihirisha nia ya kuwasaidia wananchi na pia yale manufaa ambayo tumeyaona na vile kampuni ile imeweza kupanda kutoka kiwango kimoja hadi kingine. Naamini yeye pia kuweza kuendelea kufanya kazi katika Bodi yetu ya Bunge la Kaunti hapa Mombasa itaweza kuleta manufaa vile vile katika Bunge hili. Mheshimiwa Spika mbali na uzoefu wake tumeangalia masomo yake na hii inadhihirisha kwamba ni mtu ambaye vitabu amevisoma na si kusoma tu, lakini alianza mahali pale Sheikh Khalifa alipopata C+ 1995.

Huo wakati nilikuwa nafikiri kama miaka mitano na ameweza kupanda akafanya Diploma, akaja akafanya Degree Bachelor of Commerce Finance Option, ameenda amefanya Masters na hivi sasa tunaona pia anafanya Doctor Philosophy ama PHD katika University of Nairobi mahali ambapo pia mimi nagusagusa vitabu kwa mda huu tunapoendelea kuwahudumia wananchi. Kwa hivyo huyu Bwana Swabir Masoud Abdalla naona anafaa kabisa, anatosha na anastahili kuungwa mkono ili aje hapa ajiunge na Spika wetu pamoja na Waheshimiwa walio teuliwa kutuwakilisha tusongeshe Bunge letu mbele na tuweze pia kusongesha Mombasa mbele. Mheshimiwa Spika, vile vile tukiangalia mama ambaye hapa ameteuliwa kuweza kuwakilisha wamama ama wanawake katika Bodi ile ni kwamba pia yeye tunaona masomo yake pia yanalingana na maswala yanayohusiana na fedha kwa sababu bodi hii wanasimamia fedha ambazo ni kodi ya wananchi na ambayo inafaa kutumika kwa njia ya sawa na ndio maana ukamsikia Kiongozi wa Wengi akisema kwamba hivi karibuni tumekuwa tukipata ushuhuda kutoka kwa wale wanahusika na maswala ya fedha kwamba Bunge letu limehitimu. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika bila kuongeza chumvi jamani chakula kisije kikawa chachu nasema kwamba huyu apitishwe na mimi naunga mkono kabisa. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. I now call upon the mover of the Motion to respond, Honourable Mwamwiri please respond back to your Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, chachu hutokana na vijungu kama ndimu ama limau inapowekwa katika chakula lakini uchungu unapozidi huwa chungu. Mheshimiwa Spika, nishukuru Waheshimiwa Wenza kwa kuweza kuchangia na wengi wamekuwa na mawazo chanya kuhusiana na Ripoti hii na ni matumaini yetu ya kwamba watapitishwa wawakilishi hawa wataokuwa katika Bodi ya wasimamizi wa shughuli za Bunge na Bodi hii shughuli zake ni kwa minajili ya Bunge ikiwemo wawakilishwaji lakini pia wafanyi kazi wa Bunge hili. Na tunakubaliana Mheshimiwa Spika ya kwamba katika mipango yao imesaidia kama mimi ni mara yangu ya pili lakini pia nimeweza kukua katika uwakilishaji kwa sababu chini ya Bodi hii tuliweza kupata fursa ya masomo kadha wa kadha ambayo yanahusiana na uongozi, uwakilishi lakini pia maslahi ya wananchi kule tunapotoka na pia wafanyikazi wetu katika Bunge hili. Tunao wengi waliokuja katika nafasi ya chini lakini pia wamekuwa wameweza kupata fursa ya kukua na ndio maana hatujawa na ile kuwapoteza katika halmashauri zengine bali wamesalia katika Bunge hili kwa sababu Bodi ya usimamizi ya shughuli za Bunge imekuwa ikiwaridhisha na kuwaangalia na kwamba inawapatia matumaini na pia wengi wamekuwa wakileta maombi ya kutafuta nafasi katika nafasi hii kwa sababu ni sehemu salama inayovutia na pia inaridhisha Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika ni juzi baadhi ya wawakilishi wameweza kujiunga katika Bunge hili na jinsi walivyokuja kimuonekano lakini pia jinsi walivyokuja kitajiriba na weledi sasa hivi wameweza kukua chini ya uongozi ya Mheshimiwa Spika na wale wawakilishi walikuwa katika Bodi kabla hao wengine hawajachukua nafasi rasmi. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni matumaini ya kwamba baada ya miaka mitano chini ya usimamizi wa Bodi hii, sote kwa jumla kama familia katika Bunge hili itakuwa tumeweza kukua katika majukumu yetu, katika maisha yetu lakini pia kuwapatia motisha wafanyikazi wengine kuweza kujikuza binafsi kimasomo na binafsi kinafasi na pia tuwe na baadhi kama ilivyokuwa Bunge lililopita kunaye mfanyikazi wetu mmoja Mheshimiwa Spika aliweza kupeana fursa kurudi nyanjani kujumuika na wanasiasa wengine kuomba nafasi na leo yuko hapa tofauti na mfanyikazi bali yuko hapa kama Mheshimiwa katika Bunge hili akiwakilisha kata ndogo ya Shika Adabu.

[Applause]

Na hii ni fursa ya kwamba wafanyikazi Mheshimiwa Spika, chini ya usimamizi unaostahiki inawajenga na inawapatia motisha na kuweza kukua. Kwa hayo mengi niwashukuru Waheshimiwa na kwa pamoja tuweze kupitisha Ripoti hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you the Leader of Majority even though you extended from replying to your Motion to debating and bringing up others issues. Honourable Members, I now stand to put a question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on adoption of Report on the vetting of Nominees for Members of County Assembly Service Board, representing the Public Mr. Swabir Masoud and Ms. Lynette Kamadi be adopted by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]

[Applause]

ADJOURNMENT

Thank you. Honourable Members, the House stands adjourned until Tuesday 1st August, 2023 at 10:00a.m.

The House rose at 3:25p.m.